www.tea.or.tz

# MFUKO WA ELIMU

## TEA YANADI MAFANIKIO YAKE MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA




**Toleo la 6**
**Januari - Machi**
**2025**

>> TEA YAKABIDHI MIRADI ILIYOKAMILIKA WILAYANI MTAMA NA MASASI.

>> WABUNGE WAPONGEZA UFADHILI WA MFUKO WA ELIMU KATIKA MAJIMBO YAO.

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*

# KUHUSU TEA

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharamia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

## MFUKO WA ELIMU

Mfuko wa Elimu unapokea rasilimali fedha na vifaa ambazo hukusanywa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa lengo la kufadhili miradi ya elimu nchini kutoka vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

TEA imepewa jukumu la kuhamasisha wadau mbalimbali nchini na nchi za nje kuchangia rasilimali mbali mbali kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali kuinua ubora, na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa.



## Dira

Kuwa Mfuko wa Elimu bora, wenye hadhi ya kimataifa, unaotatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



## Dhamira

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi ili kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji, usawa, ubora wa elimu na ujuzi.

# YALIYOMO


Salaam za Mkurugenzi Mkuu............................ii

TEA Yanadi Mafanikio Yake Katika Miaka Minne ya Rais Dkt. Samia..................................01

Kamati ya Kudumu ya Bunge Yaipongeza TEA kwa Utekelezaji wa Miradi ya Elimu Zanzibar...................................................................03

TEA Yakabidhi Miradi Iliyokamilika Wilayani Mtama na Masasi.....................................................05

Ufadhili wa TEA Waibua Mageuzi ya Elimu Lindi: Miradi ya Miundombinu ya Sh. Milioni 522.3 Yakabidhiwa Ruangwa na Nachingwea ..........................................................06

TEA Yaungana na Wadau Kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana Katika Sayansi........................................................07

Miradi Ya TEA Yafungua Fursa Mpya Newala, Shule Zaongezewa Usajili.......................................08

Wabunge Mkoani Njombe Wapongeza Ufadhili wa Mfuko wa Elimu Katika Majimbo Yao..........09

TEA Yaboresha Miundombinu ya Elimu Mkoani Katavi, Wanafunzi Waongezeka Shuleni.............10

Wajumbe wa Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) - Zanzibar Wafanya Ziara TEA.......11

Watumishi wa TEA Wahimizwa Kufanya Kazi kwa Ushirikiano Kuongeza Ufanisi.......................12

Wanawake wa TEA Waadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa Matendo ya Upendo.......13


## TIMU YA UHARIRI:


**Mwenyekiti**
Masozi Nyirenda

**Mhariri**
Bestina Magutu

**Wachangiaji**
Eliafile Solla
Joyce Minja


## ANUANI:


Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),
S.L.P 2516,
**Dodoma - Tanzania.**

Tovuti: www.tea.or.tz
Barua pepe: info@tea.or.tz
Instagram: officialyeatz




**Dkt. Erasmus F. Kipesha**
*Mkurugenzi Mkuu - TEA*

# SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU

Nina heshima kubwa kuwakaribisha katika toleo la sita la Jarida la Mfuko wa Elimu. Jarida hili linatoa taarifa muhimu za utendaji na mafanikio ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2024/2025 (Januari - Machi, 2025).

Katika kipindi hiki, TEA imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu nchini, kwa kuzindua na kufadhili miradi mbalimbali inayolenga kuimarisha mazingira ya kujifunzia.

Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, TEA imefanikisha utekelezaji wa miradi zaidi ya 3,700 yenye thamani ya takribani bilioni 49.5 katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Miradi hii inahusisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni, vyoo, na uboreshaji wa miundombinu mingine ya elimu, ambayo imechangia katika kuboresha mazingira ya shule na kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Katika toleo hili, tutakuletea taarifa za mafanikio ya TEA katika utekelezaji wa miradi ya elimu, ikiwemo tathmini za miradi iliyokamilika na kukabidhiwa kwa wanufaika, pamoja na ile inayotekelezwa kwa sasa.

Aidha, tutatoa picha ya mafanikio yaliyojiri katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye amekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha sekta ya elimu na kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa inayolenga kuboresha maisha ya Watanzania kupitia elimu bora.

Tunatarajia jarida hili litatoa mwanga kuhusu juhudi endelevu za TEA katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufanya elimu kuwa chachu ya maendeleo.

# TEA YANADI MAFANIKIO YAKE KATIKA MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA

Dodoma, Tanzania



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus F. Kipesha Akifafanua Jambo kwa Waandishi wa Habari.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni miongoni mwa taasisi za umma zilizopata fursa ya kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu mafanikio ya sekta ya elimu katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus F. Kipesha, alizungumza na waandishi wa habari tarehe 25 Februari 2025, ikiwa ni sehemu ya mikutano ya waandishi wa habari iliyoratibiwa na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali na Idara ya Habari - MAELEZO.

Katika mkutano huo, uliofanyika katika ukumbi wa Idara ya Habari - MAELEZO, Dkt. Kipesha alieleza kuwa TEA imefanikiwa kutekeleza miradi 3,768 yenye thamani ya Shilingi bilioni 49.5.

Dkt. Kipesha alibainisha kuwa katika kipindi hicho, TEA imefadhili ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, nyumba za walimu, mabweni, maabara za sayansi na majengo ya utawala.

Aidha, alieleza kuwa katika mwaka wa fedha wa 2024/2025, TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa imepanga kutekeleza miradi 113 yenye thamani ya Shilingi bilioni 11.3, ambayo itanufaisha wanafunzi 29,482.

*Inaendelea Uk. 02*

*Inatoka Uk. 01*

Katika utekelezaji wa miradi hiyo, TEA imepanga:

- Kujenga vyumba vya madarasa 45
- Kukarabati vyumba vya madarasa 11
- Kujenga matundu ya vyoo 336
- Kujenga nyumba za walimu 12
- Kujenga mabweni 8
- Kununua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule 9



*Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi ya Elimu, Bw. Masozi Nyirenda, akizungumza katika mkutano wa Waandishi wa Habari*

Pia, kiasi cha Shilingi bilioni 3.0 kitatumika kuimarisha miundombinu ya utoaji wa mafunzo ya amali, ikiwa ni sehemu ya kusaidia utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu nchini.

Kuhusu ushirikiano na wadau, Dkt. Kipesha alieleza kuwa katika kipindi cha miaka minne (2021/2022 – 2024/2025), TEA imepokea michango yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.11 pamoja na vifaa vyenye thamani ya Shilingi milioni 269.3 kwa ajili ya kuboresha elimu nchini.





# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YAIPONGEZA TEA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU ZANZIBAR

Unguja, Zanzibar

- *Kamati yaridhishwa na utekelezaji wa miradi ya elimu Zanzibar*
- *Miradi yenye thamani ya Sh. Bilioni 2.8 imetekelezwa*
- *Vijana 600 kutoka kaya maskini wamenufaika na Mafunzo ya Ujuzi*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imeipongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa utekelezaji makini wa miradi ya elimu, hususan inayotekelezwa Zanzibar.

Pongezi hizo zilitolewa baada ya kamati hiyo kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa na ule wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) inayosimamiwa na TEA, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2024/2025.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Florent Kyombo, alitoa pongezi hizo kwa niaba ya Kamati wakati wa ziara ya kikazi kisiwani Unguja, Zanzibar, Februari 19, 2025. Ziara hiyo ililenga kukagua na kutathmini maendeleo ya miradi ya elimu inayotekelezwa na TEA, pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Muungano katika sekta ya elimu.

“Mamlaka ya Elimu Tanzania inafanya kazi kubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu kote nchini, siyo Zanzibar pekee. Ukitembelea maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji, utaona miradi mingi ya TEA ambayo inaendelea kutatua changamoto za elimu,” alisema Mhe. Kyombo.



*Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Florent Kyombo (kulia), pamoja na Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira, Mhe. Khamis Chilo, wakifuatilia taarifa ya utekelezaji wa majukumu na miradi ya elimu upande wa Zanzibar*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ikikagua moja ya mradi wa TEA katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST).*

*Inaendelea Uk. 04*

*Inatoka Uk. 03*

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha, alieleza kuwa ndani ya kipindi cha miaka mitano, TEA imetekeleza miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.8. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 2.1 zilitumika kuboresha miundombinu ya elimu, huku Shilingi milioni 574.3 zikielekezwa katika kufadhili Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi (SDF) kwa vijana 600 kutoka kaya maskini.



*Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha akitoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria*

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya TEA Dkt. Leonard Akwilapo alisema, TEA itaendelea kutenga bajeti kila mwaka kuhakikisha miradi zaidi inatekelezwa kwa upande wa Zanzibar kama sehemu ya kuimarisha Muungano lakini pia kusaidia juhudi za Serikali za kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

**TEA ni miongoni mwa taasisi za Muungano zinazotekeleza majukumu yake Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kufadhili ujenzi wa miundombinu ya elimu, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora na yenye usawa kwa wote nchini.**



*Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Dkt. Leonard Akwilapo (kushoto), akifafanua jambo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria mara baada ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu na miradi ya elimu upande wa Zanzibar.*

# TEA YAKABIDHI MIRADI ILIYOKAMILIKA WILAYANI MTAMA NA MASASI

Masasi, Mtama

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Dkt. Leonard Akwilapo, amekabidhi vyeti kwa shule tatu zilizonufaika na miradi ya Mfuko wa Elimu wa Taifa baada ya kukamilika kwa ujenzi wake katika Halmashauri za Wilaya ya Mtama na Masasi.



Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Dkt. Leonard Akwilapo akikabidhi cheti katika hafla fupi ya kukabidhi miradi iliyotekelezwa katika Halmashauri za Mtama na Masasi Mkoani Lindi.

Dkt. Akwilapo alikabidhi vyeti hivyo wakati wa ziara yake ya kikazi kwenye halmashauri hizo, ambapo alikagua maendeleo ya miradi mbalimbali inayotekelezwa na TEA kwa ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Akizungumza na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi, Bw. James Chitumbe, Dkt. Akwilapo alisema ameridhishwa na ubora wa miradi iliyokamilika na kukabidhi vyeti hivyo kama ishara ya kuwakabidhi rasmi miradi hiyo kwa ajili ya matumizi na usimamizi.



Muonekano wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Songambele



Muonekano wa Bweni katika Shule ya Sekondari Mnara

"Katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, nitakabidhi cheti kwa ajili ya mradi wa nyumba nne za walimu katika Shule ya Sekondari Lupaso zenye thamani ya shilingi milioni 100, lakini pia shule hii ina mradi mwingine wa jengo la utawala ambalo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 80," alisema Dkt. Akwilapo.

Katika Wilaya ya Mtama, Dkt. Akwilapo alikabidhi vyeti kwa miradi ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Songambele vyenye thamani ya shilingi milioni 71.3 na bweni moja la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 katika Shule ya Sekondari Mnara lenye thamani ya shilingi milioni 142.9.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Bw. James Chitumbe, aliishukuru TEA kwa kufadhili miradi hiyo, akisema imechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha mazingira ya elimu katika shule husika.

Dkt. Akwilapo pia alitembelea miradi mingine inayoendelea kutekelezwa, ikiwemo ujenzi wa maabara ya sayansi na nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Ngongo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Lindi.

# UFADHILI WA TEA WAIBUA MAGEUZI YA ELIMU LINDI: MIRADI YA MIUNDOMBINU YA SH. MILIONI 522.3 YAKABIDHIWA RUANGWA NA NACHINGWEA

Ruangwa, Nachungwea - Lindi



*Muonekano wa nyumba nne za walimu katika shule ya Sekondari Mandarawe iliyopo Wilayani Ruangwa zilizojengwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, imekabidhi rasmi miradi ya miundombinu ya elimu yenye thamani ya Shilingi milioni 522.3 katika Halmashauri za Wilaya ya Ruangwa na Nachingwea Mkoani Lindi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia nchini.

Katika Wilaya ya Ruangwa, miradi yenye thamani ya Shilingi milioni 371.3 imekabidhiwa kwa Halmashauri hiyo, ikihusisha ujenzi wa nyumba nne za walimu katika Shule ya Sekondari Mandarawe, vyumba vya madarasa katika shule za msingi Ruangwa, Likunja na Narungombe, pamoja na matundu ya vyoo.

Hafla ya makabidhiano ilifanyika Januari 2025, ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi wa TEA, Bw. Masozi Nyirenda, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Dkt. Leonard Akwilapo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ruangwa, Bw. Frank Komba, alieleza kuwa miradi hiyo imeongeza udahili na ufaulu wa wanafunzi kwa kiwango kikubwa, huku akiahidi kuwa Halmashauri yake itahakikisha miradi hiyo inatunzwa na kutumika kikamilifu.

Katika Wilaya ya Nachingwea, TEA ilikabidhi miradi mitatu ya ujenzi wa matundu ya vyoo na madarasa yenye thamani ya Shilingi milioni 151. Miradi hiyo imefanyika katika Shule ya Msingi Stesheni, Shule ya Msingi Matangini, na Shule ya Msingi Nahimba.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nachingwea, Bw. Joshua Mnyangali, alibainisha kuwa shule zilizonufaika zimeonesha ongezeko la ufaulu kwa zaidi ya asilimia 80 kwenye mitihani ya Taifa, jambo linalowapa matumaini walimu, wazazi na jamii kwa ujumla.

Bw. Masozi Nyirenda kutoka TEA alisisitiza kuwa mamlaka itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kutafuta rasilimali zaidi kwa ajili ya kufanikisha miradi mingi ya elimu, hasa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa, kwa lengo la kuhakikisha watoto wote wanapata elimu bora katika mazingira salama na rafiki.

# TEA YAUNGANA NA WADAU KUADHIMISHA SIKU YA KIMATAIFA YA WANAWAKE NA WASICHANA KATIKA SAYANSI

Masasi, Mtama




*Watumishi wa TEA wakishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana Katika Masomo ya Sayansi (STEM) yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) iliungana na wadau wengine wa elimu nchini katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi, yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma tarehe 11 Februari 2025.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, CPA Mwanahamis Chambega, ameongoza watumishi wa TEA kushiriki katika maadhimisho hayo, ambayo yamewakutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali wanaounga mkono juhudi za kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana katika sayansi.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete, amesema kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti Ili kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika nyanja za sayansi na teknolojia.

Maadhimisho haya yanalenga kuhamasisha wanawake na wasichana kushiriki katika masomo na taaluma za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM).

Kupitia Mfuko wa Elimu, TEA imeendelea kufadhili miradi inayoboresha mazingira ya kujifunzia sayansi kwa wasichana, ili kuhakikisha fursa sawa za elimu kwa wote.

# MIRADI YA TEA YAFUNGUA FURSA MPYA NEWALA, SHULE ZAONGEZEWA USAJILI

Newala - Lindi

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kupitia ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa, imeendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia, hatua ambayo imefungua fursa mpya kwa baadhi ya shule za sekondari kupata usajili wa kutoa elimu ya kidato cha tano na sita.

Haya yalibainika wakati wa hafla ya makabidhiano ya miradi ya mabweni na matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Malocho, iliyopo Halmashauri ya Mji wa Newala. Miradi hiyo, yenye thamani ya takribani Sh. Milioni 182, ilikabidhiwa na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi wa TEA, Bw. Masozi Nyirenda, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Dkt. Leonard Akwilapo.

Mkuu wa Shule ya Malocho, Mwl. Ally Matangulu, alieleza kuwa awali shule hiyo ilikuwa na usajili wa kutoa elimu hadi kidato cha nne pekee lakini baada ya kupokea ufadhili wa TEA kwa miradi ya matundu 24 ya vyoo na bweni kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi wanafunzi 120 kwa mkupuovshule iliongezewa usajili na sasa inatoa elimu hadi kidatovcha tano.

Sh. milioni 182 zilitumika katika miradi hiyo, ambapo Sh. Milioni 40 ziligharimia ujenzi wa matundu 24 ya vyoo na Sh. Milioni 142 zilitumika kwa ujenzi wa bweni.



*Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi kutoka TEA Bw. Masozi Nyirenda akizungumza na viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Malocho iliyopo Halmashauri ya Newala Mji alipofanya ziara shuleni hapo kwa lengo la kukagua maendeleo ya miradi ya matundu ya vyoo na bweni iliyojengwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.*



*Wanafunzi wa shule ya Sekondari Malocho wakifurahi pembeni ya bweni lao lililojengwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.*

# WABUNGE MKOANI NJOMBE WAPONGEZA UFADHILI WA MFUKO WA ELIMU KATIKA MAJIMBO YAO

Njombe



*Moja ya nyumba za walimu zilizokabidhiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete.*

Mbunge wa Jimbo la Makete, Mhe. Festo Sanga, pamoja na Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, Mhe. Deo Mwanyika, wameipongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa juhudi kubwa za kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu katika majimbo yao.

Pongezi hizo zilitolewa kwa nyakati tofauti wakati wa hafla za makabidhiano ya miradi iliyofadhiliwa na TEA katika maeneo husika. Tarehe 23 Februari 2025, miradi mitano yenye thamani ya Shilingi milioni 522.7 ilikabidhiwa rasmi katika Jimbo la Makete kwa shule zinazofaidika.

Miradi hiyo imenufaisha shule tatu za sekondari na shule moja ya msingi kama ifuatavyo:

- **Shule ya Sekondari Kinyika:** Ujenzi wa madarasa matatu kwa gharama ya Shilingi milioni 71.3.

- **Shule ya Sekondari ya Wasichana Makete:** Ujenzi wa madarasa mawili Shilingi milioni 60 na maabara ya sayansi Shilingi milioni 118.1.

- **Shule ya Sekondari Lupila:** Ujenzi wa nyumba nne za walimu kwa gharama ya Shilingi milioni 201.9.

- **Shule ya Msingi Mafiga:** Ujenzi wa madarasa mawili kwa gharama ya Shilingi milioni 71.3.

Kwa upande wa **Jimbo la Njombe Mjini,** TEA imetoa ufadhili wenye thamani ya Shilingi milioni 403, ambapo miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

- Ujenzi wa matundu ya vyoo kwa Shilingi milioni 51.3, uliokamilika na kukabidhiwa kwa **Shule ya Sekondari Mpechi.**

- Ununuzi wa vifaa vya mafunzo ya amali – kilimo katika **Shule ya Sekondari Uwemba** kwa gharama ya Shilingi milioni 286.

- Mafunzo ya amali – michezo kwa Shule ya Sekondari Matola, yenye thamani ya Shilingi milioni 66.

Akizungumza na Timu ya TEA ilipotembelea jimboni humo, Mhe. Mwanyika alisema kuwa ufadhili huo unasaidia katika utekelezaji wa Sera ya Elimu inayojumuisha maarifa ya nadharia na vitendo.

Akikabidhi miradi hiyo Afisa Elimu Miradi, Bi. Consolata Mosha, alitoa wito kwa walimu na wanafunzi kuitunza miundombinu hiyo, ambayo imejengwa kwa viwango vya juu, ili iendelee kunufaisha vizazi vijavyo.

# TEA YABORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU MKOANI KATAVI, WANAFUNZI WAONGEZEKA SHULENI

Mlele, Katavi

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) inaendelea kutekeleza kwa mafanikio miradi ya uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika mikoa mbalimbali nchini. Mnamo tarehe 22 Februari 2025, TEA ilikabidhi rasmi miradi ya ujenzi wa madarasa tisa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi.

Madarasa hayo yamejengwa katika Shule ya Msingi Nsenkwa, Shule ya Msingi Kalovya, na Shule ya Msingi Ilunde kupitia ufadhili wa Shilingi milioni 202.7 kutoka Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA.

Mradi huu unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wanafunzi 300 kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia, na hivyo kuongeza motisha ya kusoma na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Kwa upande mwingine, TEA pia imekabidhi miradi mingine ya uboreshaji wa miundombinu ya shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, mkoani humo, ambapo matundu 48 ya vyoo yamejengwa katika Shule za Msingi Sibwesa na Nkungwi kwa gharama ya Shilingi milioni 80.

Mradi huu umeleta matokeo chanya, kwani wanafunzi wengi wameacha utoro na mahudhurio shuleni yameimarika.

Akikabidhi miradi hiyo Afisa Elimu Miradi Bw. Paul Kawawa aliwasihi walimu, wazazi, na jamii kwa ujumla kuhakikisha miundombinu hiyo inatumika kikamilifu kufanikisha lengo lake la kuinua elimu.

Viongozi wa kisiasa na elimu katika mkoa huo wametoa pongezi kwa TEA na uongozi wake, wakiongozwa na Dkt. Erasmus Kipesha, kwa utekelezaji madhubuti wa miradi inayolenga kuboresha elimu kwa vitendo.

Kwa ujumla, utekelezaji wa miradi hii katika mkoa wa Katavi ni ushahidi wa namna ambavyo TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, inavyotekeleza kwa vitendo dhamira ya Serikali ya kuboresha elimu kwa kuhakikisha kila mtoto anapata fursa ya kusoma katika mazingira bora na salama.




*Muonekano wa matundu 24 ya vyoo yaliyojengwa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa, Shule ya Msingi Sibwesa iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tangayika.*

# WAJUMBE WA BARAZA LA CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA) - ZANZIBAR WAFANYA ZIARA TEA

Dodoma



*Wajumbe wa Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*

Wajumbe wa Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma (IPA), wamefanya ziara ya kikazi katika Makao Makuu ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), inayosimamia Mfuko wa Elimu wa Taifa, tarehe 13 Machi 2025, kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kikazi kati ya taasisi hizo mbili.

Ujumbe wa IPA umeongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Mhe. Mmanga M. Mjawiri, akiambatana na wajumbe wengine watano, wakiwemo Mkuu wa Chuo hicho, Dkt. Shaaban Mwinchum Suleiman.

**Mikutano na Maoni ya Viongozi:**

Akizungumza katika mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Bw. Elirehema Mollel, amesema kuwa TEA iko tayari kushirikiana na IPA katika juhudi za kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Wajumbe wa IPA wameishukuru TEA kwa kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu chuoni hapo katika miaka ya nyuma, huku wakieleza matumaini yao ya kuendelea kupata ufadhili kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha, amepongeza IPA kwa utunzaji mzuri wa mradi wa TEHAMA uliowezeshwa na TEA, akisisitiza umuhimu wa kuendeleza miradi yenye tija kwa maendeleo ya elimu.

**TEA na Jukumu la Kuboresha Elimu:**

TEA ni taasisi ya Muungano inayotekeleza majukumu yake ya kuimarisha miundombinu ya elimu katika maeneo yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

# WATUMISHI WA TEA WAHIMIZWA KUFANYA KAZI KWA USHIRIKIANO ILI KUONGEZA UFANISI

Morogoro

Watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wamehimizwa kufanya kazi kwa umoja na ushirikiano ili kufanikisha malengo yaliyowekwa katika mpango kazi wa taasisi hiyo.

Ushauri huu umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi, wakati wa kikao cha nne cha baraza hilo kilichofanyika, Machi 10, 2025, mkoani Morogoro.

**Ushirikiano na Umoja:**

Akizungumza na wajumbe wa baraza hilo, Dkt. Kipesha alisisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya idara na vitengo mbalimbali ndani ya mamlaka kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji.

Alibainisha kuwa majukumu mengi ya TEA ni mtambuka, yanayohitaji ushirikiano wa karibu kati ya idara moja na nyingine, hivyo ni muhimu kwa kila mtumishi kuwa tayari kutekeleza majukumu yoyote yatakayoelekezwa kwake.

**Kikao cha Utekelezaji na Maoni:**

Katika kikao hicho, wajumbe walipitia na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka katika idara na vitengo vya mamlaka na kutoa maoni yao.




*Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Dkt. Erasmus Kipesha akisisitiza jambo wakati wa kikao cha baraza hilo kilichofanyika mkoani Morogoro*

Lengo kuu lilikuwa ni kutathmini hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na kubaini changamoto pamoja na fursa zilizopo katika kufikia malengo yake.

**Mbinu Bora za Kuboresha Utendaji:**

Aidha, wajumbe walijadili mbinu bora za kuboresha utendaji kazi wa TEA ili kuongeza tija katika sekta ya elimu. Majadiliano yalihusisha hatua zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana, pamoja na mikakati ya kuimarisha mchango wa TEA katika kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia nchini.

**Wito wa Ushirikiano na Uwajibikaji:**

Kwa kuzingatia umuhimu wa ushirikiano na uwajibikaji, Dkt. Kipesha aliwahimiza watumishi wote wa TEA kuendelea kujituma na kushirikiana ili kuhakikisha malengo ya mamlaka yanafikiwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu nchini.



*Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa TEA wakifuatilia uwasilishaji wa taarifa mbalimbali kwenye kikao kilichofanyika mkoani Morogoro*



*Kaimu Mkurugenzi Huduma za Taasisi CPA. Mwanahamis Chambega (kulia) akitoa ufafanuzi wa jambo kwa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakati wa kikao kilichofanyika mkoani Morogoro. Kushoto ni Mkaguzi Mkuu wa ndani CPA. Richard Mazinge*

# WANAWAKE WA TEA WAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI KWA MATENDO YA UPENDO

Dodoma




Wanawake wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) waliungana na wanawake wengine duniani kuadhimisha kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, ambayo huadhimishwa Machi 8 kila mwaka.

Katika kuadhimisha siku hii muhimu, wanawake wa TEA wamekutana kwa chakula cha pamoja na kubadilishana zawadi kama ishara ya mshikamano na upendo.

Kwa kuendelea kuonesha moyo wa kujali jamii, Machi 7 walitembelea Kituo cha Kulelea Watoto cha Miyuji Nyumba ya Matumaini na kutoa zawadi kwa watoto waliopo kituoni hapo, ikiwa ni njia ya kuonyesha upendo na mshikamano na watoto wenye uhitaji.

TEA inatambua mchango wa wanawake katika maendeleo ya jamii na sekta ya elimu, ikiendelea kuhimiza usawa wa kijinsia kwa mustakabali bora wa kizazi cha sasa na kijacho.







*Baadhi ya wanawake kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania, viongozi wa Kituo cha Kulelea Watoto cha Miyuji Nyumba ya Matumaini pamoja na watoto wanaolelewa katika kituo hicho wakiwa katika picha ya pamoja.*





*Baadhi ya wanawake kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania wakifurahia maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa kubadilishana zawadi kama ishara ya upendo na umoja.*

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

**S.L.P. 2516, Dodoma Tanzania.**

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*